# www.*USHUHUDAWADAKIKAMOJA*.org




## 1. RUHUSA ~ “JE, NAWEZA KUKUULIZA SWALI?”

NI KIPI KITU KIZURI ZAIDI KILICHOWAHI KUTOKEA KWAKO?

JE, NINAWEZA KUKUSHUHUDIA KITU KIZURI ZAIDI KILICHOWAHI KUTOKEA KWANGU?

## 2. K.K. ~ Elezea maisha yako KABLA YA KRISTO.

ANDIKA SIFA TATU AU MANENO MATATU:
“KATIKA MAISHA YANGU KULIKUWA NA WAKATI AMBAPO…"

1. ____________________ 2. ____________________ 3. ____________________

## 3. M.K. ~ “Ni wapi palipokuwa MAHALI pako PA KUGEUKIA?

1. ULIPATAJE KUSIKIA HABARI KUHUSU YESU? “NI WAKATI SIKU MOJA,...?

   ____________________________________________________________

2. MALIZIA SENTENSI HII: “WAKATI NILIPOELEWA KUWA YESU ALIKUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZANGU NA AKAFUFUKA TENA, NILIMKARIBISHA KATIKA MAISHA YANGU AWE …”

   ____________________________________________________________

## 4. B.K. ~ (‘Baada ya Kristo’) "Tangu nilipokutana na Kristo, Nime…”

ELEZEA MABADILIKO CHANYA, AMBAYO KRISTO AMEYAFANYA KATIKA MAISHA YAKO.

1. ____________________________________________________________

2. ____________________________________________________________

3. ____________________________________________________________

## 5. “KAMA SINGEKUTANA NA YESU…” JE, MAISHA YAKO YANGEKUWAJE BILA KRISTO?

____________________________________________________________

Use this as a MASTER COPY for you to reproduce for training others in your church and community.
© Oasis World Ministries PO BOX 58 CHAMPLIN, MN 55316 info@oasiswm.org.
No changes authorized without permission from Oasis World Ministries. V14KAT KISWAHILI - KENYA

# www.*USHUHUDAWADAKIKAMOJA*.org

**KWA KUENDELEA ZAIDI…**

Baada ya kushirikishana *USHUHUDA WA DAKIKA MOJA*™,
Unaweza ukawauliza maswali kama yafuatayo:

**“Je, naweza kukwambia jinsi Biblia inavyosema jinsi unavyoweza kuelewa unakwenda Mbinguni?”**

Kama jibu ni "ndio," waanzishie ‘KATs.’ (KUBALI, AMINI, TUBU.)

**‘K’ ~ KUBALI** nimefanya makosa, na dhambi zangu zimenitenga na Mungu Mtakatifu. (Warumi 3:23)

**‘A’ ~ AMINI** kwamba Yesu Kristo alikufa ili mimi nisamehewe, akafufuka tena, na kwamba yeye ni Mungu wa kweli. (Warumi 10:9-10)

**‘T’ ~ TUBU** kwamba nimetenda dhambi; mwombe Yesu anisaidie nijitenge mbali na dhambi na awe mwokozi wangu. (1 Yohana 1:9)

**Kama wataelewa kuhusu KATs, basi waulize swali hili muhimu:** “Ni nini kitakuzuia usiyatoe maisha yako yote kwa Yesu Kristo leo?” Kama hakuna kitu kinachowazuia, basi uliza,“Kwa msaada wa Mungu, Je utageukia mbali tokana na kile Biblia inachokiita ‘dhambi’, na kumfuata Yesu kila siku?”

---

## Shairi la Wokovu

Yesu, ulikufa msalabani
Ukafufuka kwa walopotea
Nisamehe dhambi zangu zote
Njoo uwe mwokozi wangu Bwana na rafiki
Badili maisha yangu yafanye upya
Nisaidie Bwana, nikuishie

Shairi la Wokovu.
Written by Matt and Sherry McPherson.
© 2004 by The Salvation Poem Foundation, Inc.
ALL RIGHTS RESERVED.
www.thesalvationpoem.com

## TAMBUA ZAWADI ZA BURE KWENYE: *OASISZAWADI*.ORG

**VITABU, MUZIKI & MBINU**
*ZA KUVUTIA USHUHUDA WAKO!*



**oasiszawadi.org**

---

**MALIZIA HABARI YAKO…**

Kama watasema “ndio,” basi waombe warudie maombi yao ya kimoyomoyo wakitumia ‘KATs’ uliyojifunza, au ‘Shairi la Wokovu.’ Wakisha maliza, wapongeze, na waongoze katika mambo 3: Kusoma Biblia kila siku, Kusali kila siku, na Kutafuta kanisa la kuabudia kila wiki linaloamini katika Bibilia. Badilishaneni barua pepe na namba zao za simu, fanya mawasiliano nao tena ndani ya masaa 24 kwa kuwapongeza. Wakati unapowapigia simu, waombe wakusomee Yohana 3:16-17, halafu waulize ina maana gani kwao. Waulize ni kwa jinsi gani unaweza kuwaombea, na wakaribishe mwende pamoja kanisani au kwenye kikundi chako kidogo au watie moyo kwenda kanisani jumapili inayofuatia.

SOMA ZAIDI KATIKA TOVUTI HII:
**www.frostygrapes.com**

Rafiki yangu, sasa umeandaliwa kwa ajili ya safari mpya ya milele. Muombe rafiki yako kuwa mshuhudiaji mweza kwa siku 7 zinazofuatia.Tutumie matokeo ya kazi yako kwa: info@oneminutewitness.org. Hebu tuwe washuhudiaji Wake wa kila siku… kuanzia leo!

**“MPENDWA YESU, MIMI NIPO. TAFADHALI NAOMBA UNIPATIE NAFASI YA KUWEZA KUMSHIRIKISHA MTU SIMULIZI YANGU LEO. AMINA.”**

Use this as a MASTER COPY for you to reproduce for training others in your church and community.
© Oasis World Ministries PO BOX 58 CHAMPLIN, MN 55316 info@oasiswm.org.
No changes authorized without permission from Oasis World Ministries. V14KAT KISWAHILI - KENYA